**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**

Kumb Na: NDC/PMU/3/VOL. III/06 Tarehe: 15/06/2023

# *TANGAZO LA ZABUNI*

## *MWALIKO WA KUPATA ORODHA YA MAFUNDI WA SHUGHULI ZA UJENZI WA MAJENGO MWAKA WA FEDHA 2023/2024 'LOCAL FUNDI'*

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anawatangazia wananchi wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi za ufundi wa kujenga majengo/nyumba mbalimbali za serikali kujitokeza na kuwasilisha maombi ya kuingia kwenye orodha (short list) ya mafundi kwa miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mafundi wa kawaida (Local Fundi) kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

2. Mafundi wanaohitajika ni fundi kujenga, uashi, seremala, umeme, chuma (Grill & Welding) na vioo (Aluminium).

3. Dhumuni la mwaliko huu ni kuhakikisha tunapata orodha ya mafundi wenye sifa na uzoefu ambao tutawatumia kwa utaratibu wa ushindani kwenye miradi tunayotarajia kutekeleza kwa utaratibu wa 'Force Account' kwenye maeneo yetu ya Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali, Shule za Msingi/Sekondari na Makao Makuu ya Halmashauri.

4. Shughuli za ujenzi zitahusisha mafundi waliochanganuliwa kwenye jedwali hapa chini na wawe na sifa zinazohusika:-

| LOT NAMBA | AINA YA MAFUNDI | SIFA ZINAZOHITAJIKA |
|---|---|---|
| LOT 1 | Fundi Uashi/Kujenga | i. Ajue kusoma ramani na kitafsiri<br>ii. Ajue kujenga kwa mawe na tofali<br>iii. Ajue kupiga lipu kuta za mawe na tofali |

| | | |
|---|---|---|
| | | iv. Ajue kuweka sakafu vizuri na iliyonyooka<br>v. Ajue kuweka malumalu (tiles)<br>vi. Ajue kuseti masinki ya vyoo<br>vii. Ajue kumalizia lipu (skimming)<br>viii. Ajue kutumia Zege<br>ix. Ajue michanganyo ya mota<br>x. Ajue kuchanganya saruji (cement) na mchanga<br>xi. Ajue kuweka tarazo<br>xii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya<br>xiii. Ajue vifaa vya fundi uashi |
| LOT 2 | Fundi Seremala | i. Ajue kusoma ramani<br>ii. Ajue aina za mbao<br>iii. Ajue aina za mabati ya kuezeka<br>iv. Ajue vifaa vya fundi seremala<br>v. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi |
| LOT 3 | Fundi Rangi | i. Ajue kuchanganya rangi<br>ii. Ajue matumizi ya rangi<br>iii. Ajue aina za rangi<br>iv. Ajue vifaa vya fundi rangi<br>v. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi ya upakaji wa rangi |

| | | |
|---|---|---|
| LOT 4 | Fundi Chuma (Grill & Welding) | i. Ajue kusoma ramani na kuitafsiri<br>ii. Ajue aina za vyuma na mabomba<br>iii. Ajue saizi za vyuma na mabomba<br>iv. Ajue matumizi ya vyuma na mabomba<br>v. Ajue kuchomelea na kuunganisha vyuma katika maumbo mbalimbali<br>vi. Ajue vifaa vya mafundi vyuma<br>vii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi |
| LOT 5 | Fundi Umeme | i. Ajue kuandaa mchoro wa mfumo wa umeme<br>ii. Ajue kuweka miundo mbinu ya mifumo ya umeme katika majengo<br>iii. Awe na uwezo wa kutathmini mahitaji ya vifaa vya umeme vinavyotosheleza katika kazi husika<br>iv. Awe amesajiliwa na anatambulika na TANESCO Mkoa wa Njombe |
| LOT 6 | Fundi Bomba (Plumber) | i. Awe na uwezo wa kusoma mchoro wa mfumo wa maji<br>ii. Awe na uwezo wa kutambua vifaa vyote vya bomba<br>iii. Ajue kuweka miundo mbinu ya mifumo ya maji katika majengo |

| | | |
|---|---|---|
| | | iv. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi |
| LOT 7 | Fundi Vioo (Aluminium). | i. Awe na uwezo wa kusoma vipimo<br>ii. Awe na uwezo wa kufanya kazi zenye ubora<br>iii. Awe na uzoefu wa kazi na uwezo wa kuthibitisha sehemu alizowahi kufanya kazi |

5. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi.

6. Mwombaji awe na uwezo wa kusoma ramani, kujua vitendea kazi na awe ana uzoefu wa kutosha wa shuguli za ujenzi kwenye majengo ya serikali.

7. Maombi yawe na maelezo ya kina na viambatanisho muhimu vya kazi alizowahi kufanya kwenye taasisi ya umma, kisha yafungwe vizuri kwenye bahasha na kuandikwa aina ya ufundi unaoombwa (Lot husika), yawekwe lakiri na kutumwa kwa:

**KATIBU BODI YA ZABUNI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**
**S.L.P 547**
**NJOMBE**

8. Mwombaji atalipia kiasi cha Tsh. 20,000/= (elfu ishirini tu) wakati wa kuwasilisha maombi.

9. Maombi yatakayoletwa kwa njia ya FAX, Telefax na Telegraphic system hayatapokelewa na kufunguliwa siku ya ufunguzi.

10. Mwisho wa kupokea maombi ni **ALHAMISI tarehe 22/06/2023 saa 4.00 asubuhi** na maombi na zabuni zote zitafunguliwa **saa 4.30 asubuhi** katika ukumbi **Halmashauri ya Wilaya ya Njombe , ofisi za zamani zilizopo Njombe Mjini (barabara ya Njombe – Songea karibu na Tanesco)**. Waombaji mnakaribishwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni kwa gharama zenu.

Christopher Sanga
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya - Njombe